



# UMWAGILIAJI HABARI



TOLEO LA NOVEMBA 2021

## HABARI MPYA ZA UMWAGILIAJI MWEZI HUU

### TUME KUKUSANYA BIL 30 KWA MWAKA WA FEDHA 2021-2022

#### YALIYOMO KURASA ZA NDANI

- \* Wakulima Skimu ya Magozi waifagilia Tume
- \* Maisha ya wakazi Ruaha Mbuyuni yarejea hali ya kawaida.
- \* Wakulima Mkoani Kigoma kunufaika na Mradi wa Umwagiliaji Luiche
- \* Wananchi Nanganga wakabiziwa mradi wa Bilioni Moja.
- \* Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Kilimo cha Umwagiliaji.

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imejiwekea mikakati ya kukusanya Shilingi Bilioni 30 kwa mwaka wa fedha 2021 – 2022 kwa lengo la kutunisha Mfuko wa Umwagiliaji wenye majukuamu ya kukarabati na kujenga

Miundombinu ya Skimu za Umwagiliaji nchini.

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Bw, Daudi Kaali, amesema katika kufanikisha mpango huo Tume imewaleta pamoja

wadau muhimu wa sekta ya kilimo kwa lengo la kujadiliana na hatimaye kupata mfumo bora, rahisi na wenye tija katika ukusanyaji wa tozo za umwagiliaji.

### TUME NA MIKAKATI YA KUKUSANYAJI ADA NA TOZO

Kaimu Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Bw, Daudi Kaali amewataka watendaji wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano katika zoezi la kutoa elimu pamoja na ukusanyaji wa Ada na Tozo za Umwagiliaji.

Bw, Kaali ameyasema hayo kwa nyakati tofauti jijini Dodoma huku akiamini kuwa zoezi la kuhamasisha ulipaji wa Ada na Tozo likisimamiwa vizuri Tume itapata fedha nyingi zitakazo saidia kukarabati Skimu za Umwagiliaji zilizoharibika kutokana na madhara yatokanayo

na adhari za mabadiliko ya Tabia nchi.

**“Elimu ya Ada na Tozo za Umwagiliaji ni jukumu letu sote, linahitaji uwajibikaji wa pamoja kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Wahandisi wa Umwagiliaji wa Mikoa na Wilaya kote nchini, Maafisa Kilimo katika Hal-mashauri (DAICO) pamoja na viongozi wa vyama vya Umwagiliaji ambao ndio wanaoratibu ukusanyaji wa fedha katika Skimu wanazoziongoza.”**

Aidha Kaimu Mkurugenzi Mkuu Amewaagiza Wahandisi wa

Mikoa na Wilaya kushiriki katika vipindi mbalimbali vya redio jamii zilizopo katika maeneo yao kwa lengo la kutoa elimu na kuhimiza umuhimu kwa wamwagiliaji kulipa Ada na Tozo kwa wakati kwa lengo la kuharakisha ukuaji wa sekta ya kilimo cha Umwagiliaji.



**Bw, Daudi Kaali**

Kaimu Mkurugenzi Mkuu - NIRC.



## WAKULIMA WA KIJIKI CHA MAGOZI WAISHUKURU SERIKALI

Wakulima katika Skimu ya Magozi iliyopo kata ya Ilolo Mpya Iringa Vijijini wameishukuru Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kuurejesha mto Ruaha Mdogo katika njia yake ya asili.

Kingo ya Mto Ruaha Mdogo ilivunjika na Mto kuhama kutokana na Mvua kubwa za mafuriko za Mwaka 2020 ambapo pia Mashamba ya wakulima yamejaa mchanga kutokana na kadhia hiyo.

Akizungumza na kijijini Magozi Bi, Katarina Rashid ambaye ni Mkulima katika Skimu ya Magozi, amesema maisha ya wanakijiji

wa Magozi hutegemea Zaidi kilimo cha Umwagiliaji.

Uharibifu wa Miundombinu baada ya Mafuriko ya mwaka 2020 yamesababisha maisha kuwa magumu sana na baadhi ya wakaazi kukimbilia maeneo mengine kutafuta ajira ili kupata fedha za kujikimu.

Bi, Katarina ameshukuru Serikali na kuahidi kulipa tozo za Umwagiliaji kila msimu wa mavuno kwakuwa faida ya kulipa Tozo mwenyewe binafsi ameiona mara baada ya Wataalam wa Tume

kukarabati kingo ya Mto Ruaha Mdogo iliyovunjika.

Kwa upande wake Diwani wa kata ya Ilolo Mpya Bw, Funda Mihayo amemshukuru Kaimu Mkurugezi Mkuu wa Tume Bw, Daudi Kaali kwa kuwasaidia wakulima wa Skimu ya Magozi kurekebisha Mifereji ya kupeleka Maji shambani iliyokuwa imeharika pamoja na zoezi la usanifu katika Skimu ya Liganga ambapo lengo ni kuwezesha maji kunyweshea Skimu ya Magozi na Mkombilenga. Zaidi ya Shilingi Milioni 90 zimetumika kwenye ukarabati wa Mto huu.



Lori la Tume likimwaga mawe na vifusi Wakati wa ukarabati mto Ruaha Mdogo.



Ujenzi wa Tuta Mto Ruaha Mdogo wakamilika



Mto Ruaha Mdogo

## UKARABATI MTO LUKOSI, WAKAAZI RUAHA MBUYUNI WAIFAGILIA TUME

Wakaazi wa kata ya Ruaha Mbuyuni Wilayani Kilolo mkoani Iringa wameishukuru Serikali kufuatia hatua ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kukarabati tuta la mto Lukosi lililovunjika kutokana na mvua kubwa za mafuriko zilizonyesha mkoani humo.

Akizungumza kwa niaba ya

wakaazi wa kijiji cha Ruaha mbuyuni Bw, Nasoro Kitambazi ameshukuru Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwakuwa maisha ya wakaazi wa kata ya Ruaha Mbuyuni yamerejea katika hali ya kawaida baada ya kingo ya mto Lukosi kukarabatiwa na maji kurejea katika njia yake ya asili.

Kwaupande wao baadhi ya wakaazi wa kijiji cha Ruaha Mbuyuni wamesema maisha katika kata hiyo yamerejea katika hali ya kawaida, wakaazi wa maeneo hayo wanakwenda shambani kulima, wanafunzi wanakwenda shuleni kama kawaida, na wafanya biashara wanaendelea na shughuli zao kama kawaida.



Mto Lukosi warejea katika hali yake ya kawaida



## UENDELEZWAJI WA BONDE LA LUICHE KIGOMA

Wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma hususan katika vijiji vya Kamara, Simbo, Machanzo, Nyomoli na Kasuku wanatarajia kunufaika na kilimo cha umwagiliaji kupitia mradi mkubwa wa uendelezaji wa bonde la Luiche unaotegemea kuanza mapema mwakani.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Miundombinu kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mhandisi

Mkama Kimasa amesema kuwa Serikali imeshafanya makubaliano na Serikali ya Kuwait juu ya utekelezaji wa mradi huo na eneo la Hekta Eflu Tatu ambazo zipo kwenye mkataba zinategemea kuendelezwa katika maana ya kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, na mchakato wa kutafuta mzabuni umeanza.

Mhandisi Kimasa amesema, mradi huo utagharimu kiasi

cha fedha za mkopo zaidi ya shilingi Bilioni Ishirini mpaka kumalizika.



## MRADI WA KILIMO CHA UMWAGILIAJI NANGANGA WAKAMILIKA

Wananchi wa Kijiji cha Nanganga, kilichopo katika kata ya Nanganga Wilayani Ruangwa Mkoani Lindi, wamepokea mradi wa kilimo cha Umwagiliaji, wenye thamani ya kiasi cha fedha, zaidi ya shilingi Bilioni Moja, uliojengwa na Serikali ya Awamu ya tano, kupitia Wizara

ya Kilimo chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kushirikiana na Halmashauri ya Ruangwa na fedha za ufadhili kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA).

Akiongea kwa niaba ya wananchi wa kijiji hicho baada ya makabidhiano ya mradi huo,

Diwani wa kata hiyo Shabani Kambona alisema, wamepokea mradi huo wenye jumla ya hekta 300 za umwagiliaji ambapo ujenzi wa mradi huo kwa awamu hii utawezesha Hekta 120 kumwagiliwa.

## MRADI WA ZAIDI YA SH. BILIONI MOJA NANGANGA KUKAMILIKA

Kwa upande Mwingine pamoja na kupokea mradi huo, Diwani Kambona aliiomba Serikali kumalizia kusakafia mfereji mkuu wenye urefu wa Mita Eflu Mbili (2000) ili kupunguza upotevu wa maji kwenye mifereji pamoja na kuchimba mitaro nane (8) ya kutolea maji mashambani.

Mradi wa Nanganga ni kati ya Miradi kumi na sita (16) ya SSIDP III (Small Scale Irrigation Development Project) ambapo kwa Mkoa wa Lindi imetekelezeka miradi mitatu ambayo ni wa Skimu ya Umwagiliaji Kinyope, Nanganga na Ngongowele Wilayani Newala.



Sehemu ya Miundombinu katika mradi wa Nanganga

**“Ninaishukuru Serikali yetu pendwa kwa kuleta mradi huu na nina imani kubwa sana kwa wana Ruangwa kuwa sasa ni wakati wao kujikita zaidi katika kilimo biashara na kuweza kupata chakula kutoka hapa hapa Ruangwa bila kuagiza nje ya Mkoa wetu, na kuongeza pato”**



## WADAU SEKTA BINAFSI WAZITAJA CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA HIYO

Katibu Tawala Mkoa wa Iringa Happiness Seneda ameishauri Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kutatua changamoto zinazoikabila sekta binafsi katika kikao cha Menejimenti ya Tume na wadau wa sekta binafsi mkoani Iringa kwa lengo la kutambua changamoto zinazoikabila sekta hiyo, ili tume iweze kuzifanyia kazi na kuharakisha maendeleo ya sekta ya umwagiliaji.

Seneda ameongeza kuwa endapo Menejimenti ya Tume itazifanyia kazi ipasavyo changamoto zinazopunguza kasi ya uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo cha umwagiliaji sekta hiyo itachangia ukuwajibu wa uchumi wa sekta ya Umwagiliaji kwa kasi Zaidi.



Mwenyekiti wa Bodi,  
Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

**“Ni dhahiri kwamba kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika na mbadala wa kilimo cha kutegemea mvua tulichokizoea, njia ya kiuahakikishia usalama wa chakula lakini pia ni njia ya kukuza kipato cha mkulima mojamoja na Taifa kwa ujumla**

Mwenyekiti wa Bodi Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Prof. Henry Mahoo akahitimisha kikao kazi hicho mara baada ya wajumbe kutembelea ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba dogo la mboga na matunda nje kidogo ya mji wa Iringa. Amesema ili kuharakisha maendeleo ya sekta binafsi ni muhimu kuwepo ushirikiano wa pamoja kati ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, sekta Binafsi na Halmashauri hatua itakayosaidia kutoa huduma bora kwa mkulima.

Aidha amewashauri Wahandisi wa Umwagiliaji wa Mikoa yote nchini kuandaa takwimu za Miradi yote ya Umwagiliaji katika maeneo yao ili taarifa hizo zitumike kuboresha Kanzi data ya Tume.

## TUME YANADI ELIMU YA ADA NA TOZO KATIKA KILELE CHA WIKI YA CHAKULA DUNIANI

Wataalam wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji walioshiriki katika Maonesho ya Wiki ya Chakula Duniani yaliyofanyika katika Kiwanja cha Shule ya Msingi Mandela Mjini Moshi, wameiyatumia maonyesho hayo kutoa elimu ya Ada na Tozo kwa wadau wa kilimo cha Umwagiliaji na wananchi kwa ujumla

Akitoa elimu hiyo kwa wateja waliotembelea banda la Tume, Afisa Kilimo Mwandamizi Bw, Mohamed Mcheni, amesema taratibu zote za ukusanyaji wa Ada na Tozo

zimekamilika na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

“Kwa mwaka huu wa Fedha na Miaka inayoendelea tutakusanya asilimia 5% ya mavuno kwa kila mkulima lakini pia ni muhimu kila Skimu iwe imesajiliwa Tume.

Kila Skimu inatakiwa kulipa Tsh, laki moja na Sabini na Tano. (175,000/=) ambapo Tsh, Laki Moja (100,000/=) ni Ada ya Mwaka na Shilingi Eflu Sitini (60,000) ni Ada ya Usajili na Shilingi Eflu Kumi na Tano ni Ada ya Maombi ya Usajili.



Baadhi ya Wadau wa Umwagiliaji waliotembelea banda la Tume.



## ZAIIDI YA TSH. BILIONI MOJA KUTUMIKA UPANUZI WA MFEREJI MKUU SKIMU YA KIRYA MWANGA

Wakulima katika kijiji cha KIRYA Wilayani Mwanga Mkoani Kilimanjaro wameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya Kilimo cha Umwagiliaji katika Skimu ya Mpunga ya KIRYA.

Akizungumza kwaniaba wa wakulima katika eneo la mradi Diwani wa viti Maalum Tarafa ya Lembeni Novita Mlacha amesema kukamilika kwa ujenzi wa mfereji huo kutabadili maisha ya familia katika Tarafa ya Lembeni ukizingi- atia kuwa eneo hilo linapata mvua chache, hivyo akina Mama watali- ma mazao ya aina mbalimbali iki- wemo mbogamboga na kuweza

kujikimu wao na familia zao.

Akizungumza katika eneo la mradi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mwanga Mwajuma Nasombe amewataka wanufaika wa mradi huo kuwa walenzi wa malighafi za ujenzi na miundombinu ya Umwagiliaji na waelewe kuwa Serikali inatumia fedha nyingi katika Miradi ya Umwagiliaji ili kuinua maisha ya Wananchi.

Msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Romwald Robert kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ameahidi kutekeleza wajibu wake wa kusimamia mradi huo kwa weledi na kwa matokeo chanya.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Uendelezaji Miundombinu Mhandisi Kimasa Ntonda amewataka wanufaika wa mradi huo, kutoa ushirikiano utakaohitajika kwa Mkandarasi ili kufanikisha zoezi hilo.

Zaidi ya shilingi Bilioni Moja zitatumika kuendeleza mfereji mkuu wenye urefu wa kilomita tatu, Barabara yenye urefu wa kilomita nne na nusu, pamoja na Viziba maji.

Skimu ya KIRYA ina Zaidi ya wanufaika 2000.

## IJUE KANUNI NA ADHABU YA KUTOLIPA TOZO ZA UMWAGILIAJI

Utaratibu wa kukusanya Ada na Tozo upo kisheria baada ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitisha Sheria No 4 ya Mwaka 2013 inayomtaka kila mkulima katika Skimu ya Umwagiliaji kuchangia asilimia 5% ya Wastani wa Mavuno kwa Hekari kwa Mwaka

Hivyo ndio kusema kuwa Mtu yeyote atakaye vunjia, ama kwenda kinyume na Kanuni namba 105, kama hakuna adhabu iliyotajwa mahususi anatenda kosa na baada ya kutiwa hatiani, atatakiwa kuli- pa faini ya Shilingi Milioni Moja (1,000,000/=), ama kufungwa kifungo cha Mwaka Moja jela,

ama adhabu zote mbili kwa pamoja.

**“Ewe Mkulima katika Skimu ya Umwagiliaji Lipa Tozo za Umwagiliaji kuepuka Usumbufu unaoweza kujitokeza”**





## TUME YA FUFUA KINU CHA MPUNGA MADIBIRA.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Daudi Kaali amewataka wakulima wa Skimu ya Madibira iliyopo Hal-mashauri ya Mbarali Mkoani Mbeya kutumia Ghala na Kinu cha kukoboa Mpunga mali ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kuwa Miundombinu hiyo imetengenezwa kwa lengo la kuhudumia Skimu ya Madibira

**“Napenda kuwafahamisha kuwa kinu za kukoboa Mpunga katika kituo hiki kimefanyiwa matengenezo**

**na tayari kinafaa kwa matumizi hivyo nawasihi wakulima wa skimu hii ya Madibila mtumie Miundombinu ya Ghala na Kinu, msiache haya majengo yageuke nyumba ya popo.”**

Katika hatua nyingine, Bw Kaali amesisitiza kuwa, kazi itakayofuata baada ya zoezi la kukarabati Kinu cha kukoboa Mpunga kukamilika ni pamoja na ukarabati wa majengo ya Ofisi katika kituo hicho ambayo yana nyufa kwakuwa yamejengwa miaka mingi iliyopita zikiwemo nyumba


kwaajili ya Watumishi ambazo pia zinahitaji matengenezo madogo ili zirejee katika ubora wa awali kwaajili ya matumizi ya Watumishi watacao zihitaji.

Kwa upande wao Wakulima wa Skimu hiyo ya Mbarali wameishukuru Serikali kwa matengenezo ya Kinu hicho na kuahidi kukitumia katika shughuli za kukoboa Mpunga wao pamoja na kuhifadhi katika ghala hilo.

Ukarabati wa kinu hicho unafungua upya fursa ya ajira kwa makundi mba-

limbali katika eneo hilo la Madibila wakiwemo Vijana ambao wamesema kupitia Kinu hicho watapa ajira hivyo kujiingizia kipato na kuboresha maisha yao.

Kwa mujibu wa Mhandisi Hassan Ndyali, Kinu cha Madibira kinauwezo wa kuzalisha mchele wa aina mbili, mmoja ni mchele wa kawaida ambao unaweza kutengwa katika madaraja tofauti tofauti na aina ya pili kinu hicho kinaweza kuzalisha mchele aina ya (Brown.) unaotumiwa Zaidi na wagonjwa wa Kisukari.



Ghala la Madibira

Sehemu ya Mtambo wa kukoboa Mpunga



## WAZIRI MKUU KASSIM MAJALIWA AWAAGIZA WAKULIMA WA ZABIBU SKIMU YA HOMBOLU WAITUNZE MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI.

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji  
P.O BOX 146,  
Kikuyu, Kusini.  
DODOMA

+255262962073

E-mail: [info@nirc.go.tz](mailto:info@nirc.go.tz)

**KILIMO CHA UMWAGILIAJI**  
**KILIMO CHA UHAKIKA**

[www.nirc.go.tz](http://www.nirc.go.tz)

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amewataka wakulima wa Zabibu katika Skimu ya Hombolo iliyoko nje kidogo ya jiji la Dodoma kuitunza Miundombinu ya Umwagiliaji katika Shamba hilo ili iweze kudumu kwa

muda mrefu na kuhudumia Skimu hiyo kwa tija.

Mheshimiwa Majaliwa ameyasema hayo wakati wa ziara yake katika Skimu hiyo, ambapo amejionea jitihada

zinazofanywa na wakulima katika uzalishaji wa zao hilo.

**“Kwanini Zabibu isipate mafanikio, sasa Serikali imedhamiria na Mheshimiwa rais Samia Suluhu Hassan ameagiza tusimamie ndio maana nimekuja na timu kubwa ya watendaji serikalini kila mmoja asimamie”**

Aidha Waziri Mkuu Majaliwa amewakumbusha Wakulima

wa Zabibu katika shamba hilo waepuke kurusha takataka ndani ya mifereji san-



jari na kufanya ukarabati wa mara kwa mara ili Miundombinu hiyo idumu kwa muda mrefu na kuweza kutoa huduma ya Umwagiliaji yenye tija katika uzalishaji wa zao la Zabibu.

## NIRC KUJITANGAZA KUPITIA SEKTA YA MICHEZO

Viongozi wa Baraza la Michezo wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wali-ochaguliwa katika kinyanganyiro kikali cha kugombea nafasi za Mwenyekiti na Mwenyekiti Msaidizi wa Michezo, pamoja na nafasi ya Katibu Mkuu na Katibu Mkuu Msaidizi, wameapa kukuza tasnia ya michezo katika Taasisi hiyo na kutumia fursa walioipata kutangaza shughuli za Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kupitia sekta ya Michezo.

Akizungumza baada ya uchaguzi huo Mwenyekiti aliyeshinda Bw. Yassin

Kazoba ambaye ni mchumi, ametoa ahadi ya kushirikisha Watumishi wote wa Tume katika shughuli za michezo kwani Utendaji wa kazi unategemea afya za Watumishi.

Katibu wa Baraza hilo jipya Bw. Dan-ny Makange alisema ana mkakati wa kuainisha wachezaji

katika Ofisi za Tume nchi nzima

Ili kuunda timu bora kwa baadhi ya michezo.

